

SMZ
ZANZIBAR REVOLUTIONARY GOVERNMENT
MUFTI'S OFFICE

P.O. BOX 2479
TEL: 2233788
MOBILE: 0777483627
ZANZIBAR – TANZANIA
ofisiyamuftizanzibar@gmail.com

ص.ب : 2479
هاتف : 2233788
محمول: 0777483627
زنجبار - تنزانيا



KUMB: WKS/MSZ/N.N.T/ VOL.I1/27

DATE: 19 /03/2020

**MAPENDEKEZO YA OFISI YA MUFTI JUU YA UCHUKUAJI WA
TAHADHARI YA MARADHI YA KORONA**

Mnamo tarehe 18/3/2020 Ofisi ya Mufti ilifanya kikao cha dharura kikijumuisha wajumbe wa baraza la ulamaa, kujadili hatua za tahadhari ya maradhi ya virusi vya Korona zikijumuisha mambo yafuatayo:

1. Kufunga Madrasa , Mahad, vyuo, mihadhara, madarsa ya watoto mitaani na darsa za watu wazima (yakiwemo mafunzo ya ndoa).
2. Kuepuka mikusanyiko isiyokuwa ya lazima kama vile khitma matanga arubaini na mingineyo.
3. Ubebeaji wa jeneza uwe kwa watu maalum.
4. Sherehe za harusi maholini na karamu zizuiliwe, lakini Akdi ya harusi zinaweza kuendelea kwa watu wa lazima tu.
5. Kuzuiliwa Semina zote za kidini zikiwemo za Hijja na nyenginezo.
6. Kutofanyika Mkusanyiko wa dua, rukia na visomo .
7. Swala ziendeleze za jamaa misikitini isipokuwa, kisomo cha swala , khutba na nyiradi zifupishwe.
8. Kuweka usafi wa kutosha misikitini zikiwepo na sabuni maalum za kuoshea mikono, na nivizuri watu kutia udhu nyumbani.
9. Kutopeana mikono na kukumbatiana.
10. Kuendelea kumuomba Mwenyezi Mungu atuondolee janga hili kwa Kuleta Istighfar.Kunuti katika sala zote za fardhi pamoja na dua nyenginezo za kinga .
11. Kupandisha bidhaa wakati wa shida ni katika makosa makubwa kidini.
12. Haifai kwa Muislamu kukimbia Kadari ya Mwenyezi Mungu (ni vizuri akisubiria pale alipo).
13. Wazazi wachukue nafasi ya kuwasimamia watoto wao majumbani kitaaluma katika kipindi hiki cha kufungwa skuli na madrasa.
14. Kuwajenga watu katika msingi ya Imani na kumtegemea Mwenyezi Mungu.

.....
KHALID ALI MFAUME
KATIBU WA MUFTI
ZANZIBAR

